

KARATASI YA 2
MACHI/APRILI 2019
MUDA: SAA 3
FASIHI NA MBINU ZA KUFUNDISHIA
MAAGIZO

- a) Mtihani huu una sehemu MBILI kuu: Sehemu ya A, FASIHI na sehemu ya B, MBINU ZA KUFUNDISHIA
- b) Jibu maswali matatu kutoka sehemu ya A- Swali ya kwanza ni la LAZIMA Chagua maswali mengine mawili kutoka swali la 2 au 4. Usijibu maswali mawili kutoka kwa kitabu kimoja.
- c) Andika majibu yote kwenye nafasi ulizoachiwa.
- d) Jibu maswali yote kwenye sehemu ya B

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SEHEMU	SWALI	UPEO	ALAMA
A	1	15	
	2a	15	
	2b	15	
	3a	15	
	3b	15	
B	4	15	
	5	20	
	6	20	
JUMLA			

SEHEMU A: FASIHI (ALAMA 45)

1. USHAIRI

Abdilatif Abdalla: Sauti ya Dhiki

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuatia.

Kamliwaze

Tumishi inuka hima, Utwae wangu waraka

Huko nitakokutuma, Uwenende kwa haraka

Na haya mate natema, hima yasije kauka inuka saa inuka.

Nenda kwa mwenzangu mja, kanisalimiye sana

Mwambe ni zetu, pamoja, huzuni anazoon

Mambo huenenda yakijia, ni dasituri bayana
'kipeleleza 'taona.

Nasivundikwe na moyo, kwa mambo yalotuswibu
Sisi kujikwa na hayo, si kitu kilo ajabu
Tushike tuliyonayo, tusiyawate swahibu
Nyoyo zisife kwa tabu

Kama haya 'mewajika, waliwoanza azali
Walokuwa wakitaka, haki ishinde batwili
Walifikwa na mashaka, Sampuli sampuli
Nasitusitahamili.

- i) Taja na ueleze bahari zozote mbili za shairi hili. (alama 2)
- a) _____
- b) _____
- ii) Taja istilahi mbili zinazoweza kutumika kuelezea mistari ya mwisho ya shairi hili.
(alama 2)
- a) _____
- b) _____
- iii) Taja na ufafanue mifano miwili ya inkisari katika shairi hili. (alama 4)
- a) _____
- b) _____
- iv) Eleza muundo wa ubeti wa nne wa shairi hili. (alama 4)
- v) Eleza mbinu ya kishairi iliyotumika katika maneno yafuatayo (alama 3)
- a) Kanisalimiye
- b) Nasivundikwe
- c) Dasituri

2. TAMTHILIA

Jeff mandila: Upepo wa mvua
Jibu swali la 2(a) au 2 (b)

- a) Fafanua dhima ya kidani katika kuendeleza tamthilia ya upepo wa mvua (alama 15)
- b) "Pia unipe habari urudipo, ingawa paka akiwa hakimu, panya hashindi kesi"
 - i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
 - ii) Fafanua mbinu ya lugha iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)
 - iii) Eleza sifa za mzungumzaji. (alama 9)

3. HADITHI FUPI

P.1. Iribe Mwangi na H. Babusa (Wahariri): Vazi la mhudumu.
Jibu maswali 3(a) au 3(b)

- a) i) 'Kujisaidia' ni jazanda. Eleza maana ya neno hili katika hadithi ya 'Salamu za Kushoto' huku ukitoa mifano. (alama 10)
- ii) Taja na ufafanue sifa zozote tano za profesa ndizi.
- b) Kwa kuzingatia hadithi ya 'Kura Msalani'
Jadili jinsi haki za kibinadamu zinavyokiukwa. (alama 15)

SEHEMU B: MBINU ZA KUFUNDISHIA (ALAMA 55)

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

- 4. a) Eleza umuhimu wa sehemu ya maoni katika ratiba ya mafunzo ya somo la Kiswahili.
(alama 5)
- b) Jadili makosa kumi yanayowakumba wanafunzi wanapofundishwa sarufi. (alama 10)
- 5. a) Eleza mambo matano utakayofanya ili kuwandaa wanafunzi kwa kipindi cha mjadala.
(alama 10)

- b) Taja malengo yoyote matano ya kuwa na kipindi cha mjadala. (alama 5)
- c) Taja na ueleza mambo matano ya kuzingatia unapochagua nyenzo za kufundishia katika madarasa ya chini. (alama 5)
6. Andaa somo na uonyeshe jinsi utakavyo funza msamiati wa rangi katika darasa la tatu. (alama 20)